Government of Western Australia
Department of Health
Public and Aboriginal Health Division

Mradi wa Chanjo kwa Kidato cha 8 – maelezo kwa wazazi

Kwa nini chanjo ni muhimu?

Chanjo hukinga watu dhidi ya magonjwa ya kuambukiza ambayo yana hatari kubwa ya kuumwa sana, kupata ulemavu na kifo. Chanjo inachokoza athari ya kinga inayokinga watu wasipogusana na mgonjwa tena katika mazingira.

Chanjo zote zinazopatikana sasa nchini Australia zishinde vipimo vikali vya salama kabla ya kukubaliwa. Chanjo zinafuatiliwa daima kwa usalama na kufaa. Soma zaidi kuhusu usalama wa chanjo na athari ya kawaida na ya adimu: healthywa.wa.gov.au/immunisation

Mradi wa chanjo kwa Kidato cha 8

Nchini Australia, wanafunzi wa kidato cha 8 wanapewa chanjo bila malipo kupita Mradi wa Chanjo ya Taifa kukinga dhidi ya:

* Mkamba
* Pepopunda
* Kifaduro (pertussis)
* Virusi vya papilloma vya Binadamu (HPV).

Unaweza kusoma zaidi kuhusu magonjwa haya na chanjo zinazotumiwa kukinga dhidi ya hayo kwa: healthywa.wa.gov.au/immunisation

Unahitaji kufanya nini

Furushi hii ya ruhusa ya chanjo imetolewa kwako kupitia mradi wa kidato cha 8 cha shule ya mtoto wako. Furushi ina habari na fomu ya ruhusa ndani yake.

Kama mzazi au mlezi unahitajika:

* kusoma fomu ya ruhusa na karatasi ya ukweli wa chanjo kwa uangalifu, na angalia healthywa.wa.gov. au/immunisation au wasiliana na nursi wa shule yako ukihitaji maelezo zaidi
* kuweka tiki kwenye boxi nyekundu au boxi kijani katika fomu ya ruhusa, kuonyesha chanjo zipi unazoziruhusu, na yoyote unayoacha kuruhusu, ndipo weka saini kwenye nafasi
* kutoa habari kwenye fomu ya ruhusa kuhusu matatizo ya afya yanayoweza kuathiri jibu la chanjo ya mtoto wako.
* kurudisha foma shuleni, **hata kama ukikataa chanjo**.

Labda nursi atawasiliana nawe ikiwa anahitaji habari zaidi.

Wanafunzi pekee ambao wana fomu iliyojazwa kabisa pamoja na saini watachanjwa.

Kama mtoto wako hakupokei chanjo yake kwa siku ile, utafahamishwa, na **uchaguzi badala wa chanjo utatolewa**

Kabla mtoto wako hajachanjwa

Ugonjwa mdogo wa kawaida, kama mafua na homa isiyo kali, hautachelewesha chanjo. Hata hivyo kwa hali nyingine inashauriliwa kuwa chanjo isipewa au ichelewa kwa sababu ya hali ya afya. Umwambie nursi wa chanjo au wa shule kama mtoto wako:

* amepata athari kubwa kufuata chanjo yoyote ya zamani
* amewahi kuwa na aleji kali kwa hiyo chanjo hayasifiwa
* alikuwa na chanjo hai katika mwezi uliopita (k.m. kifua kikuu, surua, homa ya manjano)
* alikuwa na sindano ya immunoglobulini au kuongeza damu nzima katika muda wa miezi mitatu iliyopita
* ana ugonjwa unaoathiri kinga ya mwili, (k.m. liukimia, saratani, HIV/ukimwi) au anatumia matibabu yanayoathiri kinga (k.m. madawa ya steroidi kama hydrokortisone au prednisolone, tibu ya eksrei, tiba ya dawa kali kwa kansa)
* anaishi na mtu ambaye ana ugonjwa unaoathiri kinga ya mwili au anayetumia matibabu yanayoathiri kinga

Kutunza baada ya chanjo

Mahali pa sindano panaweza kuwa nyekundu na kuvimba – weka kitambaa baridi chenye maji.

Labda kutakuwa na maumivu, homa, kuumwa kichwani au uchovu. Kwa kuumwa kichwani, toa paracetamol ilivyoelezwa kwenye labo. Ikiwa homa ikiendelea, zungumza na daktari.

Soma healthywa.wa.gov.au/immunisation kwa maelezo zaidi kuhusu athari za kawaida na adimu kwa chanjo.

Tafuta ushauri wa uganga mara moja kama kuna athari unayofikiri ni kali au hakutazamia.

Watoaji wote wa chanjo hapo WA wanahitajika kwa kisheria kutoa repoti athari mbaya inayofuata chanjo. Wazazi pia wanaweza kutoa repoti kuhusu athari kali yoyote baada ya chanjo mtandoni kwenye wavvs.health.wa.gov.au, au kupiga simu pale Kliniki Kuu ya Chanjo kwenye 9321 1312.

Kumbukumbu ya chanjo

Kufuata chanjo, wanafunzi watapokea kumbukumbu ya chanjo waliyopokea.

Chanjo zote zinazosimiamiwa kupitia mradi shuleni zinarekodiwa kwenye Sajili ya Chanjo ya Australia (AIR).

Kuongeza, chanjo za HPV zinarekodiwa kwenye sajili ya HPV ya Taifa: hpvregister.org.au

Mawasiliano

Kliniki Kuu ya Chanjo
Simu: 9321 1312 saa 2.30 asubuhi hadi saa 10.30 jioni (8.30am–4.30pm) siku za kazi

Daktari yako ya mtaani

Kituo cha afya ya jamii, hospitali au kituo cha afya ya umma pa mtaani,
healthywa.wa.gov.au/publichealthunits

healthdirect Australia
simu: 1800 022 222

Habari zaidi

Idara ya afya
healthywa.wa.gov.au/immunisation

Mradi wa Chanjo ya Australia
1800 671 811 au immunise.health.gov.au

Hati hii inaweza kupatikana ikiombewa kwa njia badala kwa mtu mwenye ulemavu.

Kutungwa na Kurugenzi ya Kudhibiti Magonjwa wa Kuambukiza© Idara ya Afya 2017

Haki ya kunakili ya habari hii ni ya Jimbo la Western Australia isipokuwa imeelezwa tofauti. Badala ya kutumia kwa sababu ya kusoma kibinafsi, utafiti, zungumzo au kukagua, kama inavyoruhusiwa na utoaji wa *Sheria ya Haki ya Kunakili 1968*, hakuna sehemu inayoruhusiwa kupigwa nakala au kutumiwa tena kwa sababu yoyote bila ruhusa ya maandishi ya Jimbo la Western Australia.

IMM-013031 OCT'17